



Hivi yule aliyemfanya atembea kwa miguu miwili hawezi kumfanya atembea kwa uso wake siku ya Kiyama?

Imepokelewa kutoka kwa Qatadah -Mwenyezi Mungu amrehemu amesema: Alitusimulia Anas Bin Maalik -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- kuwa Mtu mmoja alisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu vipi kafiri atafufuliwa akitembea kwa uso wake? Akasema: "Hivi yule aliyemfanya atembea kwa miguu miwili hawezi kumfanya atembea kwa uso wake siku ya Kiyama?" Akasema Qatadah: Kwa nini asiweze, ninaapa kwa utukufu wa Mola wetu anaweza kufanya hivyo.

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Aliulizwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- vipi atafufuliwa Kafiri akitembea kwa uso wake siku ya Kiyama? Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-akasema: Hivi Mwenyezi Mungu aliyemfanya atembea kwa miguu miwili hapa Duniani hawezi kumfanya atembea kwa uso wake siku ya Kiyama?! Mwenyezi Mungu ni muweza wa kila kitu.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/65068>

